

Maswali

1. Paulo alikuwa akiishi wapi?
2. Athene ilikuwa tofauti namna gani na Yerusalem?
3. Nini ilikuwa kwa mlima ulioitwa Akropoli?
4. Paulo alisimama akaangalia madhahu gani?
5. Watu wa Athene walitaka Paulo azungumze nao wakiwa wapi?
6. Paulo aliwambia Waathene kwamba atawambia juu ya Mungu yupi?
7. Paulo aliambia watu wa Athene nini kuhusu Mungu?
8. Watu wa Athene hawakuamini nini?
9. Watu wengi wa Athene waliamini Injili?
10. Kuwa na akili ni la maana kwa Mungu? Nini ndiyo ya maana kwa Mungu?

Majibu

1. Paulo alikuwa akiishi Athene.
2. Athene ilikuwa na hekalu, vihekalu na sanamu. Yerusalemu haikuwa na sanamu na ilikuwa na Hekalu moja.
3. Hekalu nyngi.
4. Madhabuhi ya mungu asiyejulikana.
5. Waliambia Paulo aseme na watu kama wamekutana kwa Kilima cha Mars
6. Mungu wasiyemjua.
7. Mungu mmoja wa kweli. Aliyeumba kila kitu. Haishi kwa hekalu, asiyetengenezwa kwa dhahabu wala kwa fedha. Mungu wetu anatupenda. Alituma Yesu aje ili akufe kwa ajili yetu.
8. Hawakuamini kwa ufulufuo wa wafu.
9. Hapana, ni wachache tu.
10. Hapana. La maana kwa Mungu ni kuwa na imani na tumpende.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



97 Paulo na mungu asiyejulikana

Kwa Biblia

Matendo ya Mitume 17: 16 – 34

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba kuna Mungu wa kweli na ni mmoja tu. Mungu hakubali watu kwa sababu ni werevu. Mungu anataka watu wenye wana imani na wanampenda

Somo

Paulo alikuwa akiishi Athene iliyoko Yunani. Athene ndio ilikuwa mji mkuu wa eneo hiyo. Ilikuwa ni kituo cha miundo tofauti ya ujuzi. Athene ilikuwa na chuo cha maana katika Ufalme wa Kirumi. Watu waliokuwa wakiishi Athene walikuwa werevu sana.



Akropoli iliyoko Athene

Paulo alisomea Yerusalem. Hakukuwa na sanamu Yerusalem. Kulikuwa na Hekalu moja Yerusalem – ya Mungu mmoja wa kweli. Athene ilikuwa tofauti sana. Katikati ya Athene kulikuwa na kilima kilichoitwa Akropoli. Juu ya Akropoli kulikuwa na hekalu nydingi. Athene ulikuwa mji mzuri. Kulikuwa na vihekalu na hekalu kila mahali.


Paulo alitembea tembea Athene. Aliudhika alipoona watu wa Athene wanaabudu sanamu. Mji huo ulijaa hekalu na vihekalu vyenye watu waliabudu na miungu ya uongo. Paulo alijua kwamba kulikuwa na Mungu mmoja pekee. Watu wa Athene hawakujuu kwamba kulikuwa na Mungu mmoja wa kweli. Badala yake waliabudu miungu wengi wa uongo.

Paulo alinyamaza, akasimama na kuangalia kwa hekalu moja. Kando ya madhabahu, ilikuwa imeandikwa, "Kwa mungu asiyejulikana." Watu wa Athene walikuwa wamejenga madhabuhu kwa kila mungu mwenye walifikiria. Walikuwa na uoga wakidhani kwamba wanaweza kuwa wamesahahu mungu moja. Mungu aliyekuwa amesahauliwa anaweza kuwakasirikia. Kwa hivyo walijenga madhabahu kwa mungu asiyejulikana.

Paulo alienda kwa Sinagogi ya Athene. Alihubiria Wayahudi. Aliwambia habari njema ya Yesu na Ufalme wa Mungu. Lakini Wayahudi hawakuwa na haja. Tena Paulo akahubiria pahali kulikuwa na soko.

Watu wa Athene walipenda kusikia mambo mageni. Walisikia Paulo akihubiria sokoni. Watu wa Athene walikaribisha Paulo aje azungumze na watu wao wa hekima. Hao watu walikaa wakijadili juu ya mambo mageni. Wale watu wa hekima walikuwa wakiwa na mikutano yao kwa Kilima cha Mars. Paulo alienda kuzungumza nao kwa hicho kilima.

Paulo aliwambia, "Watu wa Athene! Ninaona nyinyi ni watu mnaotafakari mambo ya dini. Nilikuwa nikiangalia hekalu zenu na vihekalu. Nilipata hekalu ya mungu asiyejulikana. Nitamfundisha juu ya Mungu msiyemjua."



Paulo alizungumza na watu Athene kwa Kilima cha Mars

kwa sababu yetu. Mungu anatuita tutubu na tuajane na sanamu. Mungu amechagua siku yenye atahukumu ulimwengu kuititia kwa mwanawе. Mungu alifufua Yesu kutoka kwa wafu."

Watu wa hekima walisikiliza Paulo mpaka alipofika kwa ufufuo kutoka kwa wafu. Hawakuamini kwa ufufuo. Wengi wao walimcheka.

Kulikuwa na mtu mmoja au wawili walioamini. Walibatizwa. Athene ilikuwa na watu wengi sana walikuwa na akili. Lakini hawakuamini Injili. Imani ni ya maana sana kwa Mungu kuliko kuwa na akili. Lazima tuamini kwa Mungu na tujifunze kumpenda.

Paulo aliambia watu wa hekima wa Athene, "Mungu ni Mungu wapekee wa kweli. Aliumba ulimwengu na kila kitu kilichomo. Mungu haishi kwa vihekalu wala hekalu zilizotengenezwa na watu. Mungu ni Bwana wa Mbingu na nchi. Mungu anataka watu wampende na wamwabudu. Anataka awape uzima na furaha ya milele."

Paulo alisema, "Mungu alipanga historia ya ulimwengu mzima. Yeye hufanya kazi kwa maisha ya watu. Mungu si kama sanamu anayetengenezwa kutoka kwa fedha na dhahabu. Mungu ni Baba yetu. Anatupenda. Mungu alituma mwanawе, Yesu aliyekufa